

Sheria za mifugo;

- a. Sheria ya Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya mwaka 2003 kifungu cha 43. Sheria hii inawataka wafugaji wote kupata kibali cha kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine kama ilivyoelekezwa katika sheria.
- b. Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali ya Vyakula vya Mifugo Na.13 ya mwaka 2010 kifungu cha 20. Sheria hii inawataka Wafugaji kufuga idadi ya mifugo kulingana na uwezo wa eneo la malisho.
- c. Sheria ya Usajili, Utambuzi na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010 kifungu cha 12 na 24. Sheria hii inawataka wafugaji kusajili mifugo yao kwa mujibu wa sheria husika.

Kwa kutumia sheria tajwa hapo juu hadi kufikia **Januari 30, 2018** Jumla ya ng'ombe **703,753** wamepigwa chapa ya moto kati ya ng'ombe **841,044** waliolengwa sawa na asilimia **84**.